Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.48, - 2025

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*






# AHADI ZAGEUKA VITENDO: SIKU 100 ZA RAIS SAMIA

- KAZI NA UTU TUNASONGA MBELE -

# TAHARIRI

## MKAKATI WA KKK KUCHAGIZA MAGEUZI YA ELIMU NCHINI

Mnamo Januari 29, 2026, jijini Dar es Salaam, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, alizindua rasmi Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wa Elimu ya Awali na wanafunzi wa Darasa la I na II.

Uzinduzi huu ni hatua kubwa ya utekelezaji wa ahadi za siku 100 alizotoa wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Mkakati wa KKK unalenga kuhakikisha kila mtoto anapata stadi za msingi za kusoma, kuandika na kuhesabu mapema kabla ya kufika darasa la tatu, ili waweze kujifunza kwa ufanisi zaidi katika ngazi zinazofuata za elimu.

Haya ni maono kabambe ya Mhe. Rais kuondoa dhana kwamba watoto wetu wanafika madarasa ya juu ya shule za msingi wakiwa hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu. Waswahili wanasema ugonjwa umepata mwarobaini.

Mkakati huu ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2030, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2024 (Toleo la 2023) na utekelezaji wa Agenda ya Afrika 2063 pamoja na Lengo la Nne la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG 4) linalosisitiza upatikanaji wa elimu bora kwa usawa na ujumuishi.

Hakika Tanzania haitabaki nyuma, kwani Mkakati huu unaangalia mbinu za ufundishaji, walimu, vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na miundombinu. Bila kusahau nafazi ya mzazi katika kuhakikisha mtotoi wa darasa la awali mapka la pili anamudu stadi za KKK.

Tunampongeza Rais wetu kwa maono haya, Serikali kwa kwa ujumla. Heko kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kutekeleza hili. Kwa mkakati huu macho na masikio tuelekeze kwenye utekelezaji.






BODI YA UHARIRI

Sylvia Lupembe
*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Lucas Haule
Miriam Olomy
Fradius Mugoa
Elizabeth Marwa
Dionice Lukweme
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Mkakati wa KKK >

# RAIS SAMIA ATOA MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MKAKATI WA ELIMU

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa maelekezo kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI na Wizara nyingine zinazoshughulika na elimu kuhakikisha utekelezaji kamili wa Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK).



Mhe. Samia ametoa maelekezo hayo Januari 29, 2026 jijini Dar es Salaam akizindua Mkakati huo, amesema Wizara husika lazima zihakikishe mkakati huo unatekelezwa kikamilifu katika ngazi zote ili kuleta matokeo yanayopimika na yenye manufaa kwa watoto na taifa kwa ujumla.

Aidha, ameelekeza tathmini za maendeleo zifanyike mapema ili kubaini watoto wenye changamoto na kuwapatia msaada kwa wakati, huku akisisitiza uwajibikaji wa walimu, wakuu wa shule na maafisa elimu katika kufuatilia utekelezaji wake.

Rais Samia amesema Serikali itaendelea kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Mkakati huo, kuhakikisha rasilimali na mifumo vinakwenda sambamba na matokeo yaliyokusudiwa.

Aidha, ameipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloji kwa maandalizi thabiti ya Mkakati huo, akieleza kuvutiwa na matumizi ya mbinu shirikishi za ujifunzaji zilizooneshwa wakati wa uzinduzi kwa kutumia zana na nyenzo bunifu zinazopatikana nchini.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda, ameeleza maeneo makuu ya utekelezaji wa Mkakati huo ni pamoja na kuimarisha njia za ufundishaji kupitia mafunzo endelevu kwa walimu, maandalizi ya vifaa shirikishi vya kufundishia, mapitio ya mitaala hususan masomo ya sayansi, tathmini ya mara kwa mara ya maendeleo ya wanafunzi, na ushirikishwaji wa jamii katika mchakato wa elimu.

Amesisitiza kuwa mpango huo utatekelezwa kwa miaka mitano hadi 2030, na kutakuwa na mrejesho wa kila mwaka kuonyesha hatua ilifikiwa kwa umahiri wa wanafunzi.



Samia Scholarship >




# WAZIRI MKENDA: SAYANSI NA TEKNOLOJIA NGUZO YA MAENDELEO YA TAIFA

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema kuwa sayansi na teknolojia ni nguzo kuu za maendeleo ya taifa na kwamba Serikali imejipanga kutoa fursa za masomo na mafunzo ndani na nje ya nchi kupitia programu mbalimbali.

Akizungumza Januari 30, 2026 jijini Dar es Salaam katika hafla ya kuwaaga vijana 16 wanaokwenda masomoni nchini Afrika Kusini chini ya ufadhili wa Samia Scholarship Extended DS na AI+, Prof. Mkenda amesisitiza dhamira ya Serikali kuendeleza vipaji vya sayansi kwa vijana wa Kitanzania ili kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Ametaka wazazi na wanafunzi kuzitambua fursa za masomo zinazopatikana duniani na kuhimiza wanafunzi wenye uwezo wa kitaaluma kuendeleza vipaji vyao.

Aidha, Prof. Mkenda amesema licha ya jitihada za Serikali, bado kuna changamoto ya uhaba wa walimu wenye ujuzi wa kutosha katika fani za sayansi, hivyo kunahitajika uwekezaji mkubwa katika mafunzo ya walimu ili kuhakikisha elimu bora.

Ameongeza kuwa Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kujifunza na kutoa nafasi kwa walimu kupata mafunzo ya kitaalamu ili kuendana na mahitaji ya dunia ya sasa. Pia ametoa wito kwa wadau wote, ikiwemo taasisi za elimu, kushirikiana na Serikali kusaidia wanafunzi wenye changamoto mbalimbali ili wasiachwe nyuma.

> *Dhamira ya Serikali kuendeleza vipaji vya sayansi kwa vijana wa Kitanzania*



Siku 100 za Rais Samia >

# UTEKELEZAJI WA AHADI ZA RAIS SAMIA NDANI YA SIKU 100




Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema kuwa Serikali imezindua Mkakati wa Kisayansi wa Miaka Mitano wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) wenye kauli mbiu "Elimu ya Awali Msingi wa Maendeleo Endelevu". Lengo ni kuhakikisha kila mtoto anapofikia darasa la tatu anakuwa na umahiri wa KKK.

Prof. Mkenda ameeleza hayo Januari 31, 2026 jijini Dodoma, akizungumza na Waandishi wa Habari kuhusu utekelezaji wa ahadi za Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katika siku 100 za uongozi wa Awamu ya Sita, muhula wa pili katika sekta ya elimu, sayansi na teknolojia.

"Lengo letu ni kuhakikisha kila mtoto anapofikia darasa la tatu awe na umahiri wa kusoma, kuandika na kuhesabu bila shida. Katika utekelezaji wa Mkakati huu, UNICEF wameahidi kutoa shilingi TZS Bilioni 2 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mafunzo kwa walimu.," amesema Prof. Mkenda.

Amesema Serikali imetekeleza ahadi ya kuajiri walimu 6,044 kati ya 7,000 wa sayansi na hisabati, huku taratibu za ajira kwa waliobaki zikiendelea. Aidha, shule 26 maalum za sayansi kwa wasichana na shule 5 za vipaji kwa wavulana zimekamilika, na nyingine zipo katika hatua za ujenzi.


Prof. Mkenda ameongeza kuwa Wizara kwa kushirikiana na waajiri, VETA na vyuo vikuu imeandaa mfumo wa kulinganisha mafunzo na mahitaji ya soko la ajira katika sekta za nishati, TEHAMA na viwanda, utakaotolewa Februari 9, 2026.

> **"Elimu ya Awali; Msingi wa Maendeleo Endelevu**

Sambamba na hilo, amesema kuwa ujenzi wa vyuo 64 vya VETA ngazi ya wilaya umefikia asilimia 67 na vitakapokamilika vitadahili wanafunzi 33,000 kwa mwaka.

Serikali imeongeza mikopo ya Elimu ya Juu na diploma kutoka Shilingi Bilioni 460 hadi Trilioni 1.2 kwa mwaka wa fedha 2026/27. Pia inakamilisha ujenzi wa kampasi mpya 16 za Vyuo Vikuu katika mikoa ya Kigoma, Lindi, Tanga, Tabora na Zanzibar ili kupanua fursa za elimu ya juu.

Pia, Serikali imenunua na kusambaza vifaa vya kidijitali na saidizi vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 5.35 kwa ajili ya walimu na walimu tarajali wenye ulemavu katika halmashauri 184, hatua inayolenga kuhakikisha usawa katika upatikanaji wa elimu.



Mageuzi ya Elimu >

# MAGEUZI YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KUJENGA UCHUMI IMARA NA ENDELEVU

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema kuwa Serikali imedhamiria kufanya mageuzi ya elimu, sayansi, utafiti na ubunifu ili kujenga uchumi imara na endelevu.

Mhe. Samia amesema hayo Januari 8, 2026 baada ya kuzindua Jengo la Taaluma na Utawala la Taasisi ya Sayansi za Bahari Zanzibar Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM - MSI). Amesisitiza kuwa Taasisi hiyo, ni mdau muhimu kwa Serikali katika kujenga uchumi shindani na shirikishi.

Mhe. Rais ameongeza kuwa Taasisi hiyo ya kimkakati itachangia uvuvi endelevu, utalii wa bahari na uchumi wa Bluu. Ameishukuru Benki ya Dunia kwa kushikiana na Serikali katika kutekeleza mradi wa Mradi wa HEET.

Aidha, ameipongeza Wizara ya Elimu Syansi na Teknolojia kwa kusimamai mradi wa HEET kwa ufanisi na kuleta matokeo chanya huku akiwataka vijana kutumia fursa ya kusoma kwa bidi ili kupata maarifa na ujuzi.

Amewataka Wahadhiri na watafiti kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi kuleta maendeleo, na amewahimiza wanafunzi kujifunza kwa bidii, kuwa mabalozi na walinzi wa rasilimali za bahari.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema kuwa Mradi wa HEET unajenga jumla ya majengo 1,177 ya elimu ya juu kote nchini, ikiwemo majengo mapya 130, maabara na karakana 309, mabweni na hosteli 26, maktaba, ofisi, nyumba za watumishi, zahanati na cafeteria.

Prof. Mkenda ameishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuujumuisha uzinduzi wa jengo hilo katika maadhimisho ya Miaka 62 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, akibainisha kuwa hatua hiyo inaimarisha juhudi za kuleta mageuzi katika elimu, sayansi, utafiti na ubunifu.








Elimu Maalum >

# TEKNOLOJIA ZA KIDIJITALI KUWEZESHA UJIFUNZAJI ELIMU MAALUM NA JUMUISHI

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Prof. Adolf Mkenda amesema kuwa, Serikali inaendelea na utekelezaji wa sera na maboresho ya mitaala, na kwamba jitihada za uwekezaji zimewezesha wanafunzi wenye mahitaji maalum kupata elimu bora.

Prof. Mkenda ameeleza hayo Januari 05, 2026 jijini Dodoma, akizindua ugawaji wa vifaa vya kielimu na saidizi kwa walimu, wakufunzi na walimu tarajali wenye ulemavu vyenye thamani ya Sh. Bilioni 5.3.

Waziri huyo amekumbusha alichosisitiza Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Tanzania kuwa, Serikali inapotekeleza maendeleo jumuishi, itaendeleza jitihada zilizoanza za kuweka miundombinu na vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika ngazi zote za elimu. Vifaa vilivyozinduliwa ni pamoja na kompyuta mpakato 688, mashine ya kidijiti ya kurekodi sauti 377, tabuleti 196, machine ya braille ya kielektroniki 19, emboza 6, machine ya kuongeza sauti 7 na seti 4 za kupima usikivu.

Vifaa hivyo vimesambazwa katika shule za Msingi 309, shule za Sekondari 629 na Vyuo vya Ualimu 10 kwa ajili ya waalimu, wakufunzi na walimu tarajali wenye mahitaji maalum katika halmashauri zote 184.

Kamishna wa Elimu, Dkt. Lyabwene Mtahabwa, amesisitiza kuwa msingi wa elimu ni walimu, na katika Karne ya 21 hawapaswi kuwa hodari wa kushika chaki pekee bali wanapaswa kuijua na kuitumia teknolojia kikamilifu katika ufundishaji na ujifunzaji.

Naye, Mkurugenzi wa Elimu Maalum, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Magreth Matonya, amesema walibaini walimu 1,055 wanakabiliwa na changamoto za ufundishaji, ikiwemo 342 wenye ulemavu wa viungo wasiokuwa na vifaa vya kufundishia na 310 wenye ulemavu wa uoni, usikivu, viziwi na ualbino.









# ELIMU KIDIJITALI, HITAJI SIYO CHAGUO - PROF. NOMBO



> *“Mabadiliko ya kidijitali si chaguo tena, bali ni hitaji la lazima katika elimu*

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amesema kuwa Miongozo ya Kitaifa ya Elimu ya Kidijitali kwa ngazi zote za elimu na Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Akili Unde (AI) katika Elimu inatoa mwelekeo wa namna taasisi zinavyoweza kutumia teknolojia za kidijitali na AI katika ufundishaji, utafiti, tathmini na utawala.

Prof. Nombo ameeleza hayo Januari 14, 2026 jijini Dodoma wakati akifungua Warsha ya kujenga uelewa wa pamoja juu ya Mkakati huo na Miongozo yake, akisisitiza kuwa mabadiliko ya kidijitali si chaguo tena, bali ni hitaji la lazima katika elimu, ili kuzalisha nguvu kazi mahiri.

Katibu Mkuu huyo, amewataka walimu na waelimishaji kutumia kikamilifu teknolojia katika kufundishia na kujifunzia ili kwenda sambamba na mabadiliko yanayojiri duniani katika nyanja hiyo.

“Vyuo vya ualimu, vyuo vikuu na taasisi zote za mafunzo zinapaswa kuzingatia ufundishaji wa kidijitali, ujumuishaji wa TEHAMA, uelewa wa Akili Bandia (AI), pamoja na stadi za data katika programu za mafunzo ya awali na mafunzo kazini” amesema Prof. Nombo.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi amesema kuwa, Mkakati huo pamoja na Miongozo yake, imezingatia ubora wa elimu, usawa wa fursa, ubunifu, na matumizi yanayolengwa ya teknolojia za kidijitali Nchini.

Amehimiza ushirikiano na wadau ili kufikia malengo yaliyokusudiwa katika kutekeleza Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Shule na Vyuo vya Ualimu na Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

Mingine ni Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Vyuo Vikuu na Mwongozo wa Kitaifa wa Matumizi ya Akili Unde katika Elimu.



VETA na Ajira >

# VETA MOSHI YATAKIWA KUIMARISHA USHIRIKIANO NA MAKAMPUNI KUKUZA AJIRA NA TEKNOLOJIA MPYA

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, ameielekeza VETA Moshi kuimarisha ushirikiano na makampuni na viwanda ili kuongeza ajira kwa wahitimu na matumizi ya teknolojia mpya, kwa kuzingatia uelekeo wa nchi kama ulivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, sera za kisekta na miongozo mbalimbali ya kitaifa.

Mhe. Ameir ametoa maelekezo hayo Januari 07, 2026, alipotembelea chuo hicho, akisisitiza kuwa ushirikiano huo unaboresha mafunzo na kulingana na mahitaji ya soko la ajira.

Aidha, amesema kuwa utekelezaji wa mafunzo ya sekta ya madini kupitia programu jumuishi ya ufundi wa teknolojia ya uchimbaji madini kwa kushirikiana na Chemba ya Madini Tanzania utawezesha utoaji wa mafunzo yanayoakisi mahitaji halisi ya sekta hiyo muhimu kwa taifa.

Amesema kuwa Serikali itaendelea kuwekeza katika kuongeza fursa na kuinua ubora wa mafunzo ya ufundi stadi kwa kununua vifaa vya kisasa, kuimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, pamoja na ujenzi wa vyuo vipya vya VETA 64 nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), CPA Anthony Kasore, amesema kuwa Chuo hicho, kimeendelea kushirikiana na viwanda na migodi ili kuhakikisha mafunzo yanayofundishwa yanahakisi mahitaji ya soko la ajira na kuwawezesha vijana kupata fursa za ajira kwa haraka.

Ameongeza kuwa Chuo hicho kimekuwa kivutio kwa vijana kutoka ndani na nje ya nchi, ikiwemo Comoro, Congo na Rwanda, ambao hujiunga kusomea fani mbalimbali, hali inayodhihirisha ubora na umahiri wa mafunzo yanayotolewa.



***Mhe. Wanu Hafidh Ameir***
*Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia*

Aidha, ameongeza kuwa VETA imeweka mkakati wa kuhakikisha watu wenye mahitaji maalum wanajiunga na mafunzo ya ufundi stadi bila kulipa ada. Hatua hii inalenga kuwaonyesha jamii kuwa nao wana uwezo wa kushiriki kikamilifu katika kuinua uchumi wa taifa.

Katika kuunga mkono juhudi za Serikali, katika kuimarisha ElimuAmali, Mbunge wa Moshi Mjini, Mhe. Ibrahim Shayo, ameahidi kufadhili masomo ya vijana 10 kila mwaka katika Chuo cha VETA Moshi. Amesema kuwa hatua hiyo ni fursa kwa vijana wa Mkoa huo, kujijengea ujuzi, kuboresha maisha yao na kuchangia maendeleo ya taifa.



Ujuzi na Ajira >

# UJENZI WA VETA ZA WILAYA KUIBUA ARI YA VIJANA KUPATA UJUZI NA AJIRA

Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi CCM Taifa, Fadhil Rajabu Maganya, amesema kuwa ujenzi wa vyuo vya VETA pamoja na uwekaji wa vifaa na samani za kisasa utawawezesha vijana kujifunza kwa vitendo na kupata ujuzi wa kujiajiri.

Akizungumza Januari 17, 2026 jijini Dodoma wakati wa ziara ya viongozi wa Umoja huo kukagua utekelezaji wa Ilani ya CCM, Maganya alisema ujenzi wa VETA 65 za wilaya na moja ya mkoa wa Songwe ni hatua ya kujivunia inayolenga kuongeza umahiri wa vijana ili waweze kushindana katika soko la ajira ndani na nje ya nchi.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dkt. Hussein Mohamed Omar, alisema Serikali inaendelea kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo kwa lengo la kuimarisha mafunzo ya ufundi stadi na kuwaandaa vijana kuwa wabunifu, wazalishaji na washindani katika uchumi wa kitaifa na kimataifa.

Amesema ujuzi unaotolewa katika Vyuo vya VETA ni kwa vijana wote, ngazi zote, umri wowote na kwamba ni kitu ambacho hakitoki kichwani wala mikononi akisisitiza mara unapoupata unakusaidia muda wowote na wakati wowote Ametaja eneo lingine ambalo utekelezaji wake umefanikiwa kuwa ni ujenzi wa VETA akisema katika ilani ya CCM ya Mwaka 2020-2025 wameweza kuongeza Vyuo vya ufundi Stadi takribani 33 katika Mikoa na Wilaya mbalimbali hivyo kufikia VETA 80 mwaka 2024.

Amesema ujuzi unaotolewa katika Vyuo vya VETA ni kwa vijana wote, ngazi zote, umri wowote na kwamba ni kitu ambacho hakitoki kichwani wala mikononi akisisitiza mara unapoupata unakusaidia muda wowote na wakati wowote ametaja eneo lingine ambalo utekelezaji wake umefanikiwa kuwa ni ujenzi wa VETA akisema katika ilani ya CCM ya Mwaka 2020-2025 wameweza kuongeza Vyuo vya ufundi Stadi takribani 33 katika Mikoa na Wilaya mbalimbali hivyo kufikia VETA 80 mwaka 2024.



> *"Ujuzi unaotolewa katika Vyuo vya VETA ni kwa vijana wote, ngazi zote, umri wowote*



Elimu ya Ufundi >

# SERIKALI YAENDELEA KUWEKEZA KATIKA MAFUNZO YA VYUO VYA UFUNDI STADI




> ***" Serikali itaendelea kugharamia elimu ya ufundi***

Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika elimu ya ufundi nchini ikiwemo kugharimia chakula na mafunzo kwa vitendo viwandani kwa maelfu ya wanafunzi, ili kuzalisha rasilimaliwatu yenye ujuzi unaokidhi mahitaji ya soko la ajira na kuchochea maendeleo ya Taifa.

Hayo yamesemwa Januari 8, 2026 mkoani Songwe na Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Daniel Mushi, katika Mahafali ya Kumi na Tisa (19), Duru ya Tatu (3) ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Kampasi ya Songwe.

Prof. Mushi amesema kuwa Serikali itaendelea kugharamia elimu ya ufundi katika mwaka wa fedha 2025/2026 ikiwemo kutoa huduma ya chakula kwa wanafunzi 18,316 katika taasisi mbalimbali za elimu ya ufundi nchini pamoja na kugharamia mafunzo kwa vitendo viwandani (Industrial Practical Training - IPT) kwa wanafunzi 2,085. Ameeleza kuwa jitihada hizo ni sehemu ya mkakati wa Serikali wa kuhakikisha Taifa linakuwa na wataalamu wa fani za amali wenye uwezo wa kuchachua maendeleo ya kiuchumi na kusaidia kutatua changamoto za jamii.

Akizungumza katika mahafali hayo, Prof. Mushi amewapongeza wahitimu wa Stashahada ya Uhandisi Ujenzi na wahitimu wa fani ya ufundi bomba ngazi ya pili, akisema kuwa elimu waliyoipata ni hazina kubwa kwao binafsi, familia zao na Taifa kwa ujumla.



# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

---

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

---

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi,
Muhimbili (MUHAS),
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

---

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius
Kambarage Nyerere,
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

---

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
**27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,**
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

---

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

---

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

---

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

---

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz

**- KAZI NA UTU TUNASONGA MBELE -**